

Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

Kitabu cha Pili



Islamic Propagation Centre

Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

KITABU CHA PILI

Islamic Propagation Centre

Toleo la Pili 2005

Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

©Hakimiliki 2005 IPC

Elimu ya Dini ya Kiislamu
Madrasa na Shule za Msingi
Kitabu cha pili

Wachapaji/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.
Chapisho la Pili, 13, January, 2005
Nakala 1000

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
P.O.BOX 55105, simu 022-22450069.

Usanifu wa kurasa na Jalada: Islamic Propagation Centre.
Michoro: Kati Kabatembo -Morogoro.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Neno la Awali

Shukrani zote njema anastahiki Allah (s.w). Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofuata njia yake.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa kitabu hiki cha pili kwa ajili ya watoto wetu wa Madrasa na Shule za msingi. Kitabu hiki ni katika mfululizo wa vitabu saba kwa ajili ya Madrasa zetu na shule za msingi.

Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watoto wa kiislamu kupata elimu ya msingi ya dini yao katika fani za Qur'an, Tawhid, fiqh, akhlak na tarekh.

Tunamuomba Allah atujaalie kulifikia lengo lililokusudiwa na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (s.w).

Wabillah Tawfiq

Mwalimu Mratibu
Islamic Propagation Centre

Yaliyomo

1. Somo la Kwanza :Qur'an.....	1
Kusoma na tafsiri.....	1
Zoezi la kwanza.....	29
2. Somo la Pili: Tawhid.....	30
Allah(s.w) ndiye chanzo cha Uhai.....	30
Zoezi la Pili.....	37
3. Somo la Tatu: Fiqh.....	38
Nguzo za Uislamu.....	38
Zoezi la Tatu.....	51
4.Somo la Nne: Akhlaq.....	52
Mtoto Mwema.....	52
Zoezi la Nne.....	66
5. Somo la Tano: Historia.....	67
Utume wa Muhammad (s.a.w).....	67
Zoezi la Tano.....	76

Kusoma na Tafsiri

Kusoma

Mwanafunzi wa Darasa la Pili anatarajiwa aweze kusoma kwa ufasaha na kuhifadhi sura katika Juzuu Amma kuanzia **At'-Twaariq** mpaka **An-Nabaa**.

Tafsiri

Pamoja na kuhifadhi, mwanafunzi wa darasa la pili anatarajiwa ajue tafsiri ya sura za Juzuu Amma kuanzia Al-Faatiha mpaka Al-A'laa.

Makka

Suratul Fatiha (1)

ina aya 7

1. Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwenye Kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

2. Sifa zote njema zinamstahikia Allah. Bwana na mlezi wa viumbe vyote.

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ①

3. Mwingi wa Rehma, mwenye kurehemu.

الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ②

4. Mwenye kumiliki siku ya malipo.

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ③

5. Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ④

6. Tuongoze katika njia iliyonyooka.

اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ⑤

7. Njia ya wale uliowaneemesha, sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea.

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ
الْبَغْضَوِّ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ⑥

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1.Sema, Najikinga kwa Bwana mlezi wa watu.

2.Mfalme wa watu.

3.Muabudiwa wa Watu.

4.Na shari ya mwenye kutia wasiwasi, mwenye kurejea nyuma.

5.Atiaye wasiwasi nyoyoni mwa Watu.

6.(Ambaye) ni katika majini na watu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۝

مَلِكِ النَّاسِ ۝

إِلَهِ النَّاسِ ۝

مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ۝

الَّذِي يُوسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ۝

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ۝

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1.Sema Najikinga kwa Mola wa Ulimwengu wote.

2.Na shari ya alivyoviumba.

3.Na shari ya giza la usiku liingiapo.

4.Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni.

5.Na shari ya hasidi anapohusudu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ۝

مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ۝

وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ۝

وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ۝

وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ۝

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

- 1.Sema, Yeye ni Allah moja (tu).
- 2.Allah tu ndiye anayestahiki kukusudiwa.
- 3.Hakuzaa wala Hakuzaliwa.
- 4.Wala hana anayefafanana naye hata mmoja.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ①

اللَّهُ الصَّمَدُ ②

لَمْ يَلِدْهُ وَلَمْ يُولَدْ ③

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ④

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

- 1.Pana kuangamia mikono miwili ya Abu-lahab! Naye ameshakwisha angamia.
- 2.Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma.
- 3.(Atakapokufa) Ataingia moto wenye mwako (mkubwa kabisa).
- 4.Na mkewe mchukuzi wa kuni (za fitina).
- 5.(Kana kwamba) Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayechukulia kuni za fitina hizo).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ①

مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ②

سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ③

وَأَمْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ④

فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ⑤

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Itakapofika nusura ya Allah (s.w) na kushinda.

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ۝

2. Na utakapowaona watu wakiingia katika dini ya Allah makundi makundi.

وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ۝

3. Basi hapo mtakase Mola wako pamoja na kumsifu, Umuombe msamaha, hakika yeye ndiye apokeaye toba.

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ إِنَّكَ كَانَ تَوَّابًا ۝

Kwa jina la Allah (s.w) Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Sema, Enyi makafiri.

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ۝

2. Siabudu Mnachoabudu.

لَا أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ۝

3. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.

وَلَا أَنْتُمْ عِبُدُونَ مَا أَعْبُدُ ۝

4. Wala sitaabudu mnachoabudu.

وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَا عَبَدْتُمْ ۝

5. Wala nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu.

وَلَا أَنْتُمْ عِبَادُونَ مَا أَعْبُدُ ۝

6. Nyinyi mna dini yenu nami nina dini yangu.

لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ۝

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1.Hakika tumekupa kheri nyingi.

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ۝١

2.Basi Swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili yake).

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ۝٢

3.Hakika adui yako ndiye atakaekuwa mkiwa (atakatikiwa na kila kheri).

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ۝٣

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1.Je, Unamjua yule anayekadhibisha dini (asiyeamini malipo ya Akhera)?

أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالْإِيمَانِ ۝١

2.Huyu ni yule anayemnyanyasa yatima.

فَذَلِكَ الَّذِي يَدُعُّ الْيَتِيمَ ۝٢

3.Wala hajihimizi (yeye wala wengine) kuwalisha maskini.

وَلَا يَحْضُرْ عَلَى طَعَامِ الْمَسْكِينِ ۝٣

4.Basi adhabu itawathubutikia wanaoswali.

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ۝٤

5.Ambao wanapuuza (Maamrishi) ya Swala zao.

الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ۝٥

6.Ambao hufanya riyaa.

الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ۝٦

7.Nao hunyima misaada.

وَيَسْتَعُونُ الْبَاعُونَ ۝٧

Kwa jina la Allah (s.w) mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.

1. Ili kuwafanya Makurayshi waendeleo.

2. Waendeleo na Safari zao za wakati wa kusi (kwenda Yemen) na wakati wa kaskazi (kwenda Shamu).

3. Basi nawamuabudu Bwana wa nyumba hii (Al-Kaaba).

4. Ambaye anawalisha (wakati Waarabu wenzao wamo) katika njaa, na anawapa amani (wakati wenzao wamo) katika khofu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ۚ قُرَيْشٌ ۙ

الْفِهْمُ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ۚ

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ۙ

الَّذِي أَطْعَمَهُم مِّنْ جُوعٍ ۖ وَآمَنَهُم

مِّنْ خَوْفٍ ۝۴

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1. Je! Huoni jinsi Mola wako alivyowafanya watu wenye ndovu?

2. Je! Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika?

3. Na tukawapelekea ndege makundi kwa makundi.

4. Wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuchoma.

5. Akawafanya kama majani yaliyoliwa (yakatapikwa).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ۙ

الَّذِينَ جَعَلْنَا كَيْدَهُمْ فِي تَضَلُّلٍ ۙ

وَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ۙ

تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ سِجِّيلٍ ۙ

فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ۝۵

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1. Adhabu kali itamthibitikia kila mwenye kuramba kisogo, msengenyaji.

2. Ambaye amekusanya mali na kuyahesabu.

3. Anadhani ya kuwa mali yake yatandumisha milele.

4. Hasha! Bila shaka atavurumizwa katika (moto unaoitwa) Hutama.

5. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) ni nini Hutama?

6. (Huo) ni moto wa Allah uliowashwa (kwa ukali barabara).

7. Ambao unapanda nyoyoni.

8. Hakika huo (moto) watafungiwa (wawemo ndani yake).

9. Katika magogo marefu marefu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ۝١

الَّذِي جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ۝٢

يَحْسَبُ أَنَّ مَالَهُ أَخْلَدَهُ ۝٣

كَلَّا لَيُنْبَذَنَّ فِي الْحُطَمَةِ ۝٤

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْحُطَمَةُ ۝٥

نَارُ اللَّهِ الْمُبْقَدَةُ ۝٦

الَّتِي تَطَّلِعُ عَلَى الْإِفْكِ ۝٧

إِنَّهَا عَلَيْهِمْ مُّوَصَّدَةٌ ۝٨

فِي عِمَدٍ مُمَدَّدَةٍ ۝٩

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1. Naapa kwa zama (wakati).

2. Kuwa binaadamu yumo katika hasara.

3. Ila wale walioamini na wakafanya mema. Wakahusiana haki na wakausiana kushikamana na subira.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالْعَصْرِ ۝١

إِنَّ الْإِنْسَانَ لِفِي خُسْرٍ ۝٢

إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ۝٣

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Kumekughafilisheni kutafuta wingi (wa vitu vya ulimwengu).

أَلْهَكُمُ التَّكَاثُرُ ۝١

2. Hata mumeingia makaburini (hamjafanya lolote la Akhera yenu).

حَتَّى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ۝٢

3. Sivyo, karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo).

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ۝٣

4. Kisha (nasema) sivyo hivyo, karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo).

ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ۝٤

5. Sivyo hivyo, lau kama (nyinyi) mmajua kwa ujuzi wa yakini (kuwa sivyo hivyo, basi msingefanya hivyo).

كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ ۝٥

6. Hakika mtauona moto.

لَتَرَوُنَّ الْجَحِيمَ ۝٦

7. Kisha (nasema) mtamuona kwa yakini.

ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِينِ ۝٧

8. Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo ya neema (mlizopewa mlizitumiaje).

ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ

النَّعِيمِ ۝٨

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

- 1.(Msiba) ugongao nyoyo.
- 2.(Msiba) ugongao nyoyoni ni upi huo?
- 3.Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukaujua) ni upi huo (msiba) ugongao nyoyo?
- 4.Siku ambayo watu watakuwa kama madumadu (watoto wa nzige) waliotawanywa.
- 5.Na milima itakuwa kama sufi zilizo chambiwa (zikiwa zinapeperuka).
- 6.Basi yule mizani yake itakayokuwa mizito.
- 7.Huyo atakuwa katika maisha yanayopendeza.
- 8.Na yule ambaye mizani yake itakuwa nyepesi.
- 9.Huyo mashaka yake katika (huo moto) Hawiya.
- 10.Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) ni nini hiyo Hawiya?
- 11.Ni moto uwakao kwa ukali (kweli kweli).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْقَارِعَةُ ①

مَا الْقَارِعَةُ ②

وَمَا أَذْرُبُكَ مَا الْقَارِعَةُ ③

يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ

الْبَثْوِثِ ④

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ⑤

فَأَمَّا مَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ ⑥

فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ ⑦

وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ⑧

فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ⑨

وَمَا أَذْرُبُكَ مَا هِيَ ⑩

نَارُ حَامِيَةٍ ⑪

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1. Naapa kwa (farasi) wanaokwenda mbio wakihema.

2. Na wakitoa moto kwa kupiga kwato (chini).

3. Wakamshambulia wakati wa asubuhi.

4. Wakarusha mavumbi (makubwa) wakati huo.

5. Na wakaingia kati ya kundi (la maadui kupigana).

6. Kwa hakika binaadamu amkanusha Mola wake.

7. Naye anajua haya.

8. Na ana mapenzi makubwa kabisa ya kupendeza mali.

9. Je, hajui kuwa watafufuliwa waliomo makaburini.

10. Na kuwa yatadhihirishwa yaliyomo vifuani.

11. Kuwa Mola wao atawajua sana siku hiyo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالْعِدِيثِ صَبْحًا ①

فَالْمُورِيَّتِ قَدْحًا ②

فَالْمُغِيرَاتِ صُبْحًا ③

فَأَثَرُنَ بِهِ نَقْعًا ④

فَوْسَطِنَ بِهِ جَمْعًا ⑤

إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُودٌ ⑥

وَإِنَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكَ لَشَهِيدٌ ⑦

وَإِنَّهُ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ ⑧

أَفَلَا يَعْلَمُ إِذَا بُعْثِرَ مَا فِي الْقُبُورِ ⑨

وَ حُصِّلَ مَا فِي الصُّدُورِ ⑩

إِنَّ رَبَّهُم بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيرٌ ⑪

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1. Na itakapotetemeshwa ardhi mtetemesho wake (huo mkubwa).

2. Na itakapotoa ardhi mizigo yake.

3. Na binaadamu akasema (wakati huo) “(Oh) ina nini (leo ardhi)?”

4. Siku hiyo itatoa habari zake (zote).

5. Kwani Mola ameifunulia (ameiamrisha kufanya hivyo).

6. Siku hiyo watu watatoka (makaburini) Vikundi – vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao.

7. Basi anayefanya mema (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake.

8. Na anayefanya uovu (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ①

وَأُخْرِجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ②

وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا لَهَا ③

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ④

بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَى لَهَا ⑤

يَوْمَئِذٍ يَصُدُّ النَّاسُ أُمَّتَاتَهُ لِيُرَوْا

أَعْمَالَهُمْ ⑥

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ⑦

وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ⑧

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.

1. Wale waliokufuru miongoni mwa watu wa kitabu na washirikina (waliotoa ahadi kuwa) hawataacha (waliyonayo) mpaka iwajie hoja (iliyodhahiri ya kuonyesha upotevu wa dini zao).

2. Ni Mtume aliyetoka kwa Allah a n a y e w a s o m e a k u r a s a zilizotakazwa.

3. Ndani yake mnasharia madhubuti.

4. Wala hawakufarikiana wale waliopewa kitabu ila baada ya kuwajia hoja hiyo (waliyokuwa wakitaka).

5. Na wala hawakuamrisha ila kumuabudu Allah kwa kumtakasia dini, waache dini za upotofu na wasimamisha sala na kutoa Zakat hiyo ndiyo dini iliyo sawa (ambayo wao wameikataa).

6. (Basi) bila shaka wale waliokufuru miongoni mwa watu waliopewa Kitabu na washirikina wataingia katika moto wa Jahannam wakae humo humo milele, nao ni waovu wa viumbe.

7. Hakika wale walioamini na kutenda mema basi hao ndio wema wa viumbe.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ
الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفَكِينَ حَتَّى
تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ۝

رَسُولٌ مِّنَ اللَّهِ يَتْلُو صُحُفًا مُّطَهَّرَةً ۝

فِيهَا كُتِبَ قِيمَةٌ ۝

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِنْ
بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَةُ ۝

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ
لَهُ الدِّينَ ۝ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ
وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ وَذَلِكَ دِينُ الْقِيمَةِ ۝

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ
وَالْمُشْرِكِينَ فِي نَارِ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا
أُولَئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ۝

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
أُولَئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ ۝

8. Malipo yao kwa Mola wao ni mabustani ya daima ambayo mito inapita mbele yake wakae humo milele (hali ya kuwa) Allah amewaridhia nao wameridhika. (malipo) hayo ni kwa yule anayemuogopa Mola wake.

جَزَاءُ لَهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتُ عَدْنٍ
تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا
أَبَدًا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ
ذَلِكَ لِمَنْ خَشِيَ رَبَّهُ ۝

Makka

Suratul Qadr (97)

ina aya 5

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Hakika tumeiteremsha (Qur-an) katika usiku wenye heshima kubwa (usiku wa mwezi wa Ramadhani).

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ۝

2. Na jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) nini huo usiku wa Lalatul qadr?

وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ۝

3. Huo usiku wa hishma (huo) ni bora kuliko miezi elfu.

لَيْلَةُ الْقَدْرِ خَيْرٌ مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ ۝

4. Huteremka Malaika na Roho (za viumbe watakatifu) katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo.

تَنْزِيلُ الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ
مِنْ كُلِّ امْرٍ ۝

5. Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya Al-fajiri.

سَلَامٌ هِيَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ الْفَجْرِ ۝

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1.Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba.

2.Umemuumba mwanaadamu kwa 'alaq.

3.Soma, na Mola wako ni Karimu sana.

4.Ambaye amemfundisha kwa (msaada) wa kalamu.

5.Amemfundisha mwanaadamu chungu ya mambo aliyokuwa hayajui.

6.Sivyo hivi! Kwa hakika binaadamu hutakabari.

7.Akijiona amepata utajiri!

8.Bila shaka marejeo (ya watu wote) ni kwa Mola wako (tu).

9.Je! Umemuona yule anayemkataza?

10.Mja (wa Mungu) asiswali?

11.Je! Umemuona kama yeye yuko juu ya uongofu (kwa kufanya hivyo)?

12.Au anaamrisha wema (kwa kufanya hivyo)?

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ①

خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ②

اقْرَأْ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ③

الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ④

عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑤

كَلَّا إِنَّ الْإِنْسَانَ لِكَفْرٍ ⑥

أَنْ رَأَاهُ اسْتَعْتَبَ ⑦

إِنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ الرُّجْعَىٰ ⑧

أَرَأَيْتَ الَّذِي يَنْهَىٰ ⑨

عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰ ⑩

أَرَأَيْتَ إِنْ كَانَ عَلَىٰ الْهُدَىٰ ⑪

أَوْ أَمَرَ بِالتَّقْوَىٰ ⑫

13. Je, unaonaje kama yeye anakadhibisha na kurudi nyuma?

14. Je! Hajui ya kuwa Allah (s.w) anamuona?

15. Sivyo hivyo (anavyofanya) kama haachi, tutamkokota kwa nywele za utosi (wake tumtie motoni).

16. Utosi Muongo, wenye madhambi.

17. Basi na awaite wanachama wenzake (wamsaidie).

18. Na sisi tutawaita malaika wa motoni (wamuadhibu).

19. Sivyo! Usimtii (mbaya huyo) bali sujudu na uwe karibu na Mola wako).

أَرَأَيْتَ إِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى ۖ

أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ اللَّهَ يَرَى ۖ

كَلَّا لَئِنْ لَمْ يَنْتَهِهِ لَنَسْفَعًا بِالنَّاصِيَةِ ۖ

نَاصِيَةٍ كَاذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ۖ

فَلْيَدْعُ نَادِيَهُ ۖ

سَنَدْعُ الزَّبَانِيَةَ ۖ

كَلَّا لَا تَطَّعُهُ وَاسْجُدْ وَاقْتَرِبْ ۙ

Makka

Suratut Tyn(95)

ina aya 8

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1. Naapa kwa Tini na Zaituni

2. Na kwa mlima Sinai.

3. Na kwa mji huu (wa Makka) wenye amani.

4. Bila ya shaka tumemuumba mwanaadamu kwa umbo lililo bora kabisa.

5. Kisha tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
وَالَّتَيْنِ وَالزَّيْتُونَ ۙ

وَطُورِ سَيْنَاءَ ۙ

وَهَذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ۙ

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ
تَقْوِيمٍ ۙ

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ۙ

6. Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha, (unaoendelea maisha).

إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ۝

7. Basi ni lipi likupalo kukadhibisha malipo baada (ya kuona hayo)?

فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالذِّينِ ۝

8. Je! Allah si Hakimu muadilifu kuliko Mahakimu wote?

أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمَ الْحَكِيمِينَ ۝

Makka

Suratun Nashrah(94)

ina aya 8

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Je, hatukukupanulia kifua chako.

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ۝

2. Na tukakuondolea mzigo wako (mzito).

وَوَضَعْنَا عَنْكَ وِزْرَكَ ۝

3. Uliovunja mgongo wako?

الَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ۝

4. Na tukatukuza utajo wako?

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ۝

5. Basi kwa hakika baada ya dhiki (huja faraji.

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ۝

6. Hakika baada ya dhidi huja faraja.

إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ۝

7. Basi ukisha maliza (kulingania) shughulika kwa Ibada nyingine.

فَإِذَا فَرَغْتَ فَانصَبْ ۝

8. Na jipendekeze kwa Mola wako.

وَالِإِلَىٰ رَبِّكَ فَارْغَبْ ۝

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma,
Mwenye kurehemu.

1.Naapa kwa mchana.

2.Na kwa usiku unapotanda.

3.Hakukuacha Mola wako wala hakukukasirikia (ewe Nabii Muhammad).

4.Na bila shaka (kila) wakati ujao (utakuwa) bora zaidi kuliko uliotangulia.

5.Na Mola wako atakupa mpaka uridhike.

6.Je, hakukukuta yatima akakupa makazi (mazuri ya kukaa)?

7.Na akakukuta hujui kuongoza njia, akakuongoza?

8.Na akakukuta fakiri akakutajirisha?

9.Basi usimuonee Yatima.

10.Wala usimkaripie aulizaye.

11.Na Neema ya Mola wako usimulie (kwa kushukuru na kufanya amali njema).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
وَالضُّحَىٰ ①

وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ②

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ③

وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ④

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ⑤

أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ⑥

وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ⑦

وَوَجَدَكَ عَائِلًا فَأَغْنَىٰ ⑧

فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ⑨

وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ⑩

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ⑪

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1.Naapa kwa usiku ufunikapo (kila kitu).

2.Na kwa mchana uangazapo.

3.Na kwa aliyeumba kiume na kike.

4.Kuwa mali zenu ni mbalimbali (na jaza yenu itakuwa mbalimbali).

5.Yule anayetoa (zaka, sadaka, na vinginevyo) na kumcha Allah.

6.Na kusadiki jambo jema na (akalifuata).

7.Tutamsahilishia njia ya kuendea peponi.

8.Na afanyaye ubakhili, asiwe na haja ya viumbe wenzake.

9.Na akakadhibisha mambo mema (asiyafanye).

10.Tutamsahilishia njia ya kwendea motoni.

11.Na mali yake hayatamfaa atakapokuwa (motoni).

12.Ni juu yetu (kuwabainishia viumbe) mwongozo wa maisha.

13.Na ni yetu sisi akhera na Dunia.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى ۝

وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّى ۝

وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْأُنثَى ۝

إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّى ۝

فَأَمَّا مَنْ آعطَى وَآتَقَى ۝

وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَى ۝

فَسَنِيْرُهُ لِلْيُسْرَى ۝

وَأَمَّا مَنْ بَخِلَ وَاسْتَغْنَى ۝

وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَى ۝

فَسَنِيْرُهُ لِلْعُسْرَى ۝

وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ۝

إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَى ۝

وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَى ۝

14. Basi nakuhadharisheni na moto uwakao (kwa nguvu).

فَأَنْذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّى ۝١٤

15. Hatauingia ila muovu.

لَا يَصِلُهَا إِلَّا الْآشَقَى ۝١٥

16. Anayekadhibisha na kuipa mgongo (hii dini ya haki).

الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلَّى ۝١٦

17. Na ambaye ataepushwa nao.

وَسَيَجْزِيهَا الْآتِقَى ۝١٧

18. Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa.

الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّى ۝١٨

19. Na hali ya kuwa hakuna yeyote aliyemfanyia ihsani ili awe amemlipa.

وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزَى ۝١٩

20. Isipokuwa (anafanya haya) kwa kutaka radhi za Mola wake.

إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلَى ۝٢٠

21. Basi atapata la kumridhisha.

وَلَسَوْفَ يَرْضَى ۝٢١

Makka

Suratush Shams(91)

ina aya 15

Kwa jina la Allah, mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa jua na kwa muangaza wake.

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ۝١

2. Na kwa mwezi unapoliandama.

وَالْقَمَرِ إِذَا تَلَّهَا ۝٢

3. Na mchana unapolidhihirisha.

وَالنَّهَارِ إِذَا جَدَّهَا ۝٣

4. Na kwa usiku unapolifunika.

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ۝٤

5. Na kwa mbingu na kwa aliyezijenga.

وَالسَّمَاءِ وَمَا بَنَاهَا ۝٥

6. Na kwa ardhi na aliyezitandaza.

وَالْأَرْضِ وَمَا طَعَمَهَا ⑥

7. Na kwa nafsi na aliyeitengeneza.

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ⑦

8. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake.

فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ⑧

9. Bila shaka amefaulu aliyetakasa (nafsi yake).

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّاهَا ⑨

10. Na bila shaka amejihasiri aliyeiviza (nafsi yake).

وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ⑩

11. Kina Thamudi walikadhibisha kwa sababu ya upotofu (upotevu) wao.

كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِطَغْوَاهَا ⑪

12. Aliposimama muovu wao mkubwa (ili kumchinja huyo ngamia wa miujiza).

إِذِ انبَعَثَ أَشْقَاهَا ⑫

13. Hapo Mtume wa Allah aliwaambia, "(Huyu) ni ngamia wa Allah (muacheni) na kinywaji chake.

فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ نَاقَةَ اللَّهِ وَسُقْيَاهَا ⑬

14. Lakini walimkadhibisha (huyo Mtume, Nabii Saleh) na wakamuua (huyo ngamia), kwa hiyo Mola wao, aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na akawafuta kabisa.

فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ ⑭

رَبُّهُمْ بِذُنُوبِهِمْ فَسَوَّاهَا ⑭

15. Wala haogopi matokeo yake.

وَلَا يَخَافُ عُقْبَاهَا ⑮

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

1.Naapa kwa mji huu wa (Makka).

2.Nawe utashuka (utateremka) katika Mji huu.

3.(Na naapa) kwa kila kilichozaa na kile kilichozaliwa.

4 . K u w a t u m e m u u m b a mwanaadamu katika taabu.

5. Je! Anadhani ya kuwa hakuna yeyote atakayeweza (kumtia mkononi)?

6.Anasema, Nimeharibu mali nyingi (kwa ajili ya kuupinga Uislamu).

7.Je! Anadhani yakuwa hakuna yeyote amuonaye?

8.Je, hatukumpa macho mawili?

9.Na ulimi na midomo miwili?

10. Na tukambainishia zote njia mbili (iliyo njema na iliyo mbaya)?

11. Je! Ameukata huo Mlima, (njia nzito ya kumfikisha peponi).

12. Na nini kitakachokujulisha huo mlima (njia ya kukufikisha peponi).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

لَا أُقْسِمُ بِهَذَا الْبَلَدِ ۝

وَأَنْتَ حِلٌّ بِهَذَا الْبَلَدِ ۝

وَوَالِدٍ وَمَا وَلَدٌ ۝

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي كَبَدٍ ۝

أَيَحْسَبُ أَنْ لَنْ يَقْدِرَ عَلَيْهِ أَحَدٌ ۝

يَقُولُ أَهْلَكْتُ مَالًا لُبَدًا ۝

أَيَحْسَبُ أَنْ لَمْ يَرَهُ أَحَدٌ ۝

أَلَمْ نَجْعَلْ لَهُ عَيْنَيْنِ ۝

وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ۝

وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ۝

فَلَا اقْتَحَمَ الْعَقَبَةَ ۝

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْعَقَبَةُ ۝

13. (Kuukata mlima huo) ni kumpa mtumwa uungwana.

فَكَرَبَةٍ ۝١٣

14. Au kumlisha siku ya njaa.

أَوْ اطْعَمْتُ فِي يَوْمٍ ذِي مَسْغَبَةٍ ۝١٤

15. Yatima aliyejamaa.

يَتِيمًا ذَا مَقْرَبَةٍ ۝١٥

16. Au masikini aliye hohye hahe.

أَوْ سَكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ ۝١٦

17. Kisha awe miogoni mwa walioamini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ ۝١٧

18. Hao ndio watu wa upande wa kheri.

أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ ۝١٨

19. Lakini waliokanusha Aya zetu, hao ndio watu wa upande wa shari.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا هُمْ أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ۝١٩

20. Moto uliofungiwa (kila upande) utakuwa juu yao.

عَلَيْهِمْ نَارٌ مُّؤَصَّدَةٌ ۝٢٠

Makka

Suratul Fajr(89)

ina aya 20

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa alfajir.

وَالْفَجْرِ ۝١

2. Na kwa masiku kumi.

وَلَيْالٍ عَشْرِ ۝٢

3. Na kwa "Shafii na Witiri"

وَالشَّفْعِ وَالْوَتْرِ ۝٣

4. Na kwa usiku unapopita.

وَالنَّيْلِ إِذَا يَسْرِ ۝٤

5. (Naapa nasema) kuwa kuna katika haya (kuonekana) kiapo kwa mwenye akili.

هَلْ فِي ذَلِكَ قَسَمٌ لِذِي حَجْرِ ۝٥

6. Je! Hakuona jinsi Mola wako alivyowafanya adi (Iram).

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ۝

7. (Adi) Iram (waliokuwa) wanamajumba marefu marefu.

إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ۝

8. Ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji (mingine).

الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِي الْبِلَادِ ۝

9. Na Thamudi waliochonga majabali (wakayafanya majumba) katika uwanja (wao).

وَتَمُودَ الَّذِينَ جَابُوا الصَّخْرَ بِالْوَادِ ۝

10. Na firauni mwenye majumba kama vigingi.

وَفِرْعَوْنَ ذِي الْأَوْتَادِ ۝

11. Ambao walifanya maovu katika miji.

الَّذِينَ طَغَوْا فِي الْبِلَادِ ۝

12. Kisha walizidisha humo mambo maovu?

فَاكْتَرُوا فِيهَا الْفُسَادَ ۝

13. Kwa hivyo Mola wao aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu.

فَصَبَّ عَلَيْهِمُ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ۝

14. Hakika Mola wako yuko katika malindizo.

إِنَّ رَبَّكَ لِبِالْحَرِّ صَادٍ ۝

15. Lakini mwanaadamu, Mola wake anapomfanyia mtihani akamtukuza na kumneemesha, basi husema, "Mola wangu amenitukuza".

فَأَمَّا الْإِنْسَانُ إِذَا مَا ابْتَلَاهُ رَبُّهُ فَأَكْرَمَهُ ۝

وَنَعَّمَهُ ۝ فَيَقُولُ رَبِّي أَكْرَمَنِ ۝

16. Na anapomfanyia mtihani akampunguzia riziki yake, husema; "Mola wangu amenidhalilisha.

وَأَمَّا إِذَا مَا ابْتَلَاهُ فَقَدَرَ عَلَيْهِ رِزْقَهُ ۝

فَيَقُولُ رَبِّي أَهَانَنِ ۝

17. Sivyo hivyo bali nyinyi hamuwatazami mayatima kwa jicho la huruma.

كَلَّا بَلْ لَا تَهْتَدُونَ الْيَتِيمَ ۝

18. Wala hamjihimizi kulisha maskini.

وَلَا تَحْضُونَهُ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿١٨﴾

19. Na mnakula urithi kwa ulaji wa pupa.

وَتَأْكُلُونَ التَّرَاثَ أَكْلًا لَتًّا ﴿١٩﴾

20. Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi.

وَتُحِبُّونَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿٢٠﴾

21. Sivyo hivyo (kumbukeni) itakapovunjwa ardhi vipande vipande.

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢١﴾

22. Na kufika (amri ya) Mola wako na Malaika safusafu.

وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٢﴾

23. Basi siku hiyo italetwa Jahannamu. Siku hiyo Mwanaadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?

وَجَاءَ يَوْمَئِذٍ بِجَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ
وَأَنَّى لَهُ الذِّكْرَىٰ ﴿٢٣﴾

24. Atasema, "Laiti ningelitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo).

يَقُولُ لِيَأْتِيَنِي قَدْ مَتَّ لِحَيَاتِي ﴿٢٤﴾

25. Basi siku hiyo hataadhibu yoyote namna ya kuadhibu kwake (Allah).

فَيَوْمِئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابَهُ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾

26. Wala hatafunga yeyote jinsi ya kufunga kwake (Allah).

وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُ أَحَدٌ ﴿٢٦﴾

27. Ewe nafsi yenye kutua!

يَا أَيُّهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾

28. Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika na Allah aridhike na wewe.

ارْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾

29. Basi ingia katika kundi la waja wangu wazuri.

وَأَدْخُلْنِي فِي عِبَادِي ﴿٢٩﴾

30. Uingie katika pepo yangu.

وَأَدْخُلْنِي جَنَّاتِي ﴿٣٠﴾

Makka

Suratul Ghashiya(88)

ina aya 20

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Je! Imekuwasilia habari ya msiba utakaowafudikiza (viumbe)?

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ﴿١﴾

2. Nyuso siku hiyo ni zenye kudhalilika.

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَاشِعَةٌ ﴿٢﴾

3. Ni zenye kufanya kazi ngumu kabisa (huko motoni) zichoke.

عَائِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٣﴾

4. Waingie katika moto uwakao kweli kweli.

تَصَلَّىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٤﴾

5. Watanyweshwa (humu) katika chemchem zilichemkazo barabara.

تُسْقَىٰ مِنْ عَيْنٍ آنِيَةٍ ﴿٥﴾

6. Hawatakuwa na chakula isipokuwa cha miba.

لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيْعٍ ﴿٦﴾

7. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.

لَا يَسْتَمِنُونَ وَلَا يُغْنِي عَنْهُمْ جُوعُهُمْ ﴿٧﴾

8. Nyuso (nyingine) siku hiyo ni zenye kumemetuka.

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ ﴿٨﴾

9. Zitakuwa radhi kwa ajili ya amali zao.

لَسَعِيهَا رَاضِيَةٌ ⑩

10. Zitakuwamo katika pepo iliyotufu.

فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ⑪

11. Hazitasikia humo yasiyo na maana.

لَا تَسْمَعُ فِيهَا لَآغِيَةً ⑫

12. Humo mna chemchem zinazotiririka (kwa vizuri).

فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ⑬

13. Humo mna viti vya fahari vilivyoinuka juu.

فِيهَا سُرُرٌ مَّرْفُوعَةٌ ⑭

14. Na glasi zilizowekwa (vizuri).

وَأَكْوَابٌ مَوْضُوعَةٌ ⑮

15. Na mazulia yaliyotankdikwa vizuri.

وَمَنَارِقٌ مَّصْفُوفَةٌ ⑯

16. Na matakia yaliyopangwa safusafu.

وَزُرَائِقٌ مَبْثُوثَةٌ ⑰

17. Je! Hawatazami ngamia jinsi alivyoubwa?

أَفَلَا يَنْظُرُونَ إِلَى الْإِبْرَةِ كَيْفَ خُلِقَتْ ⑱

18. Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa?

وَالِى السَّمَاءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ⑲

19. Na milima jinsi ilivyothubutishwa?

وَالِى الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ⑳

20. Na ardhi jinsi ilivyotandazwa?

وَالِى الْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ㉑

21. Basi kumbusha, hakika wewe ni mkumbushaji (tu).

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ㉒

22. Wewe si mwenye kuwateza nguvu.

لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ㉓

23. Lakini anayerudi nyuma na kukufuru.

إِلَّا مَنْ تَوَلَّى وَكُفِّرْ ۝

24. Allah (s.w) atamuadhibu adhabu iliyo kubwa.

فِيَعَذِّبُهُ اللَّهُ الْعَذَابَ الْأَكْبَرَ ۝

25. Hakika marejeo yao ni kwetu.

إِنَّ الْبِنَاءَ لِأَيْبَهُمْ ۝

26. Kisha bila shaka, hisabu yao ni juu yetu.

ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُمْ ۝

Makka

Suratul A'alaq(87)

ina aya 20

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1.Litukuze jina la Mola wako aliyemtukufu.

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ۝

2.Aliyeumba (kila kitu) na akakitengeneza.

الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّى ۝

3.Na akakikadiria (kila kimoja jambo lake) na akakiongoza.

وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَى ۝

4.Na aliyeotesha ndisha (malisho).

وَالَّذِي أَخْرَجَ الْمَرْعَى ۝

5.Kisha akaifanya mikavu yenye kupiga weusi.

فَجَعَلَ عُثْمَانَ أَخْوَى ۝

6.Tutakusomesha wala hutasahau.

سُنُقِرُكَ فَاَلَا تَنسَى ۝

7.Ila akipenda Mwenyezi Mungu; Yeye anajua yaliyodhahiri na yaliyofichikana.

إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ۝

8.Nasi tutakusahilishia (kuitangaza) dini iliyo nyepesi (Uislamu).

وَيُسِّرُكَ لِلْيُسْرَى ۝

9.Basi waidhisha ikiwa utafaa waadhi.

فَذَكِّرْ إِنْ نَفَعَتِ الذِّكْرَى ۝

10. Bila shaka atakumbuka mwenye kumuogopa Allah (s.w).

سَيِّدًا كَرُمًا يَخْشَى ۝١٥

11. Na mwingi wa mateso atajitenga mbali nayo hayo (mawaidha).

وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَى ۝١٦

12. Ambaye atauingia moto mkubwa.

الَّذِي يَصِلُ النَّارَ الْكُبْرَى ۝١٧

13. Kisha humo hatakuwa wala hatakuwa hai.

ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَى ۝١٨

14. Hakika amekwishafaulu aliyejitakasa na mabaya.

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ۝١٩

15. Akakumbuka jina la Mola wake na akaswali.

وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ۝٢٠

16. Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia.

بَلْ تُؤْثِرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۝٢١

17. Hali ya kuwa ya akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu.

وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ وَأَبْقَى ۝٢٢

18. Hakika haya (mnayoambiwa humu katika Qur-an) yamo katika vitabu vilivyotangulia.

إِنَّ هَذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَى ۝٢٣

19. Vitabu vya Ibrahim na Musa (na wengineo).

صُحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى ۝٢٤



Zoezi la Kwanza

1. Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kuandika tafsiri ya aya

	قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ①
	قُلْ يَأَيُّهَا الْكٰفِرُونَ ②
	لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ④
	إِيَّاكَ تَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ④ ط
	فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ④ ل
	الَّذِينَ هُمْ يُرَآءُونَ ⑤
	وَيَمْنَعُونَ الْبَاعُونَ ⑦
	وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَارْغَبْ ⑧

2. Andika aya za Qur'an kwa kiarabu, zenye tafsiri ifuatayo:

- (i) Hakika amekwishafaulu aliyejitakasa na mabaya.
- (ii) Akakumbuka jina la Mola wake na akaswali.
- (iii) Wala hamjihimizi kulisha maskini.
- (iv) Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi.
- (v) Je! Ameukata huo Mlima, (njia nzito ya kumfikisha peponi).
- (vi) (Kuukata mlima huo) ni kumpa mtumwa uungwana.
- (vii) Au kumlisha siku ya njaa.
- (viii) Au masikini aliye hohye hahe.

Allah ndiye chanzo cha uhai

Mimea


Hili ni ua la plastiki. Ua hili limetengenezwa na fundi mtengeneza maua. Ua la plastiki si ua la kweli. Ni mfano wake.

Ua la plastiki halina uhai.

Ua lisilo na uhai halikui wala halifi.

Ua la kweli lina uhai. Ua lenye uhai linakuwa na linazaa. Ua lenye uhai likikatwa linakauka.

Je, ni nani aliyelipa ua uhai? Fundi wa kutengeneza maua ya plastiki hawezi kutoa uhai. Hawezi kuyapa uhai maua aliyoyatengeneza.




Nani basi anayetoa uhai kwa mimea? Allah ndiye anaipa mimea uhai. Allah ndiye chanzo cha uhai wa mimea



Wanyama

Wanyama wamezaliwa, wanakula, wanakua na wanakufa. Wanyama wanatembea. Hivyo wanyama wana uhai.

Aliyetengeneza sanamu hii ni mchonga vinyago. Sanamu la paka halina uhai. Halikuzaliwa bali limetengenezwa. Sanamu halili chakula wala halifi.



Mchonga vinyago hana uwezo wa kutoa uhai, ndio maana vinyago vyake havina uhai. Nani aliyempa paka uhai?



Bila shaka aliyeuumba wanyama ndiye aliyewapa uhai. Aliyeumba wanyama ni Allah. Allah ndiye anayewapa wanyama uhai.

Watu

Sanamu la mtoto halina uhai. Limetengenezwa likianguka chini halilii. Halisikii njaa.

Hivyo sanamu halina uhai. Watengeneza vinyago hawana uwezo wa kutoa uhai kwa vinyago vyao. Mwenye uwezo wa kutoa uhai ni yule aliyewaumba binaadamu.



Mtoto huyu ana uhai. Akifurahishwa anacheka. Akichukizwa analia. Allah ndiye aliyewaumba binaadamu. Allah ndiye aliyewapa binaadamu uhai.

Leo tumejifunza habari kubwa za kuisisimua. Tumejifunza kuwa: Mimea ina uhai. Wanyama wana uhai. Binaadamu wana uhai.

Pia tumejifunza kuwa: Aliyeipa mimea uhai ni Allah. Aliyewapa wanyama uhai ni Allah. Aliyewapa binaadamu uhai ni Allah.

Hakika Allah ndiye chanzo cha uhai. Allah amekipa uhai kila kilicho hai. Kweli Allah ndiye chanzo cha uhai. Qur-an inatufahamisha:

تَبْرَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾
الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ

Ametukuka yule ambaye mkononi mwake umo ufalme (wote) Naye ni mwenye uwezo juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai.... (Qur-an, 67:1-2).

ALLAH ANASTAHIKI KUSIFIWA NA KUSHUKURIWA

Tunampenda baba. Baba ni mtu mzuri sana. Baba anatupenda. Anatununulia chakula kizuri. Ametununulia nguo nzuri za shule na madaftari.

Kweli baba ni mtu mzuri. Tunampenda baba na tunamshukuru sana kwe vitu alivyotununulia.

Tunampenda sana mama yetu. Mama ndiye aliyetuzaa na kutulea kwa huruma. Mama hutupikia chakula kizuri sana.




Mama anatufulia nguo zetu. Hakika mama anatulea vema. Mama ni mtu mzuri sana.



Tunamshukuru sana mama kwa kutulea vizuri. Baba na mama wameumbwa na Allah.

Baba na mama wamepewa uhai na Allah. Wamepewa uwezo wa kutulea vizuri na Allah.

Chakula kizuri anachotununulia baba kimepatikana kwa uwezo wa Allah. Baba ametujengea nyumba nzuri tunamoishi kwa uwezo wa Allah.



Aliyemjaalia mama na kumjaza huruma na mapenzi juu yetu ni Allah. Allah ni mwenye uwezo zaidi kuliko baba na mama. Allah anatupenda zaidi kuliko baba na mama.

Allah anatumhuria zaidi kuliko baba na mama. Baba na mama wanampenda Allah. Wanamshukuru sana kwa neema zote

alizowaneemesha. Na sisi tunampenda Allah. Tunamshukuru sana Allah kwa kutuumba, kutupa akili na kutuumbia wazazi wazuri.

Sote tunatakiwa tumshukuru sana Allah. Allah ametuumba na kutupa uhai. Allah ndiye aliyetuneemesha kwa kila tulichonacho. Waislamu tunampenda sana Allah.

Tunamshukuru sana Allah kwa neema zote alizotuneemesha. Waislamu hushukuru Allah kwa kusema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ①

Shukurani zote anastahiki Allah Bwana Mlezi wa walimwengu wote. (1:2)

ALLAH ANASTAHIKI KUTIIWA

Mtoto mzuri huwatii wazazi wake. Akitumwa na baba yake hutekeleza. Akiitwa na mama yake huenda haraka.



Tunamtii mama kwa sababu ametuzaa, ametulea, anatumikia chakula na kutufulia nguo zetu.


Tunamtii baba kwa sababu ndiye mzazi wetu. Ndiye aliyejenga nyumba tunamokaa. Ndiye anayetununulia chakula na nguo. Ndiye anayetununulia nguo za shule na madaftari.

Baba ndiye anayetulipia karo ya shule, hatuna budi kumtii baba. Tunawaheshimu kaka na dada. Wametuzidi umri. Tunawaheshimu watu walio tuzidi umri kwa sababu wanatuzidi Maarifa. Wanafahamu mambo mengi tusiyoyafahamu. Mtoto mwenye heshima huwatii wakubwa zake.

Baba anamtii Allah. Anafuata yale Allah aliyeyaamrisha na anaacha yale Allah aliyoyakataza. Mama anamtii Allah. Anaswali kila siku mara tano. Na anafunga mwezi wa Ramadhani.

Kaka na dada nao wanamtii Allah. Wanavaa vizuri kama anavyopenda Allah. Wanaswali swala tano kila siku.

Nami pia namtii Allah. Ninawatii wazazi wangu na ninawatii wakubwa zangu. Ninaswali kila siku mara tano. Ninajiepusha na yale aliyonikataza Allah.



Sote tunamtii Allah. Tunaswali swala tano kila siku kwa nyakati zake.



Kila Muislamu wa kweli anamtii Allah. Anaswali swala tano kwa nyakati zake. Anatoa zaka, anafunga, anaacha yale yote aliyokataza Allah.

Anawahurumia wengine na anaishi nao kwa wema.

Allah anawapenda wanaomtii. Qur'an Inatufunza tumtii Allah. Inasema:

أَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَوَلَّوْا عَنَّهُ وَ أَنْتُمْ
تَسْمَعُونَ

Mtiini Allah na Mtume wake, wala msijiepushe naye hali mnasikia (8:20)



Zoezi la Pili

1. Nani ndiye chanzo cha uhai?
Chanzo cha uhai ni.....
2. Ua lisilo na uhai halina.....wala
3. Ua lenye uhaina
4. Nani anayetoa uhai kwa mimea na wanyama?
Anayetoa uhai kwa mimea na wanyama ni.....
5. Wanyama wamezaliwa,, na
6. Nani aliyeumba mauti na uhai?
Aliyeumba mauti na uhai ni
7. Tunampenda baba kwasababu anatumunulia chakula kizuri,.....
na
8. Tunampenda mama kwasababu ndiye aliyetuzaa na,
hutupikia..... nanguo zetu.
9. Nani anayetupenda zaidi kuliko baba na mama?
Anayetupenda zaidi kuliko baba na mama ni.....
10. Sisi tunampenda na kumshukuru sana Allah (s.w)
kwa.....,, na.....
11. Kila muislamu wa kweli humtii Allah (s.w) kwa
 - (i).....
 - (ii).....
 - (iii).....
 - (iv).....



Nguzo za Uislamu

Nguzo za Uislamu ni tano. Tunafahamishwa katika hadithi ifuatayo kuwa: Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema:

بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ: شَهَادَةٌ
أَنَّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ،
وَأِقَامَ الصَّلَاةِ، وَإِيتَاءَ الزَّكَاةِ، وَحَجَّ الْبَيْتِ،
وَصَوْمَ رَمَضَانَ

“Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano kushuhudia kuwa hapana Mola ila Allah na kushuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah; kusimamisha swala; kutoa Zakat; kufunga ramadhani na kuhiji nyumba takatifu (Al-Ka’aba) kwa mwenye uwezo”. (Bukhari na Muslimu).

Hadithi hii inatufunza kuwa Uislamu hauwezi kusimama mpaka Waislamu watekeleze kwa ukamilifu yafuatayo:

1. Kutoa shahada mbili kwa dhati.
2. Kusimamisha swala tano.
3. Kutoa Zakat kwa kila mwenye mali.
4. Kufunga ramadhani.
5. Kuhiji nyumba takatifu (Al-Ka’aba) kwa kila mwenye uwezo.

SHAHADA MBILI

Kutoa shahada mbili ni kusema:



أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُهُ

Ninashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.

Muislamu aliyemshuhudia Allah (s.w) kwa dhati hufuata maamrishi yote ya Allah (s.w) na kuacha makatazo yake yote.

Akijua kuwa Allah (s.w) amemuamrisha jambo fulani hulitekeleza haraka haraka kwa moyo mkunjufu. Hali kadhalika akijua kuwa Allah (s.w) amemkataza kufanya jambo fulani huliacha mara moja bila ubishi.


Muislamu aliyemshuhudia Mtume Muhammad (s.a.w) kwa dhati hutekeleza yale yote aliyotuagiza Mtume (s.a.w) na kuacha yale yote aliyotukataza.

Pia Muislamu wa kweli hujitahidi kuigiza mwenendo wa Mtume. Akijua kuwa Mtume alikuwa akifanya jambo fulani, huwa mwepesi wa kuiga jambo lile.

KUSIMAMISHA SWALA

Nguzo ya pili ya Uislamu ni kusimamisha swala tano. Swala tano anazopaswa Muislamu azisimamishe kila siku ni:

1. Adhuhuri.
2. Alasiri.
3. Magharibi.
4. Isha.
5. Alfajiri (Subhi).




Twahara

Muislamu anayekusudia kwenda kuswali hana budi kujitwaharisha. Mwili wake unatakiwa uwe safi, awe na udhu na nguo zake zisiwe zenye najisi.

Ili muislamu awe twahara, ni lazima ngozi ya mwili wake pamoja na nguo zake :

1. visiwe na mkojo au kinyesi cha mtu au mnyama.
2. visiwe vina damu, usaha na matapishi.
3. Visiwe vimepakazwa **bia** au kumwagikiwa na pombe ya aina yoyote.
4. Visiwe vimerambwa au kunuswa na mbwa ama nguruwe; au kugandwa na kitu chochote kinachotokana na wanyama hawa.



Kutwaharisha Najisi ndogo

Najisi ya (1) hadi ya (9) huitwa najisi ndogo. Najisi ndogo hutwaharishwa kwa maji safi. Katika kuondosha najisi ndogo tunaiosha sehemu yenye najisi mpaka rangi na harufu ya najisi viondoke.

Wasichana wanatwahaisha shungi



MUHIMU: Ukitwahaisha nguo yenye najisi usichanganye kwenye besini bali miminia maji.

Kutwahaisha Najisi kubwa:

Najisi ya Mbwa na nguruwe huitwa najisi kubwa. Inaitwa najisi kubwa kutokana na uzito wake katika kuitwahaisha.

Sehemu iliyopatwa na najisi kubwa hutwahaishwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:

1. Isafishe sehemu iliyoingiliwa na najisi kubwa kama unavyoondoa najisi ndogo.
2. Sugua sehemu iliyonajisika kwa udongo safi.
3. Kisha ioshe sehemu hiyo kwa maji mara tano au zaidi.

Ukifanya hivyo utakuwa umeondoa najisi hiyo kwa makosho makubwa saba:

Josh la kwanza ni lile la kuondoa harufu na rangi ya najisi.


Josh la pili ni lile la kusugua kwa udongo safi.

Josho la tatu hadi la saba yatakuwa makosho ya kumiminia maji na kusugua sehemu iliyokuwa na najisi kubwa, kosho moja baada ya jingine mpaka yatimie saba.

Muhimu: Mwalimu awaonyeshe wanafunzi namna ya kutekeleza jambo hili kwa matendo.

Kutawadha

Ni kutia udhu kwa maji safi.



Dua baada ya kutawadha

Baada ya kukamilisha Udhu Mtume (s.a.w) ametuelekeza kuelekea Qibla na kuleta dua ifuatayo:



أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ
لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا
عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah aliye mmoja tu, asiye na mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake.



لِلَّهِمَّ اجْعَلْنِي مِنَ التَّوَّابِينَ وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ وَاجْعَلْنِي
مِنْ عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ أَشْهَدُ
أَنَّ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إِلَيْكَ

Ee Allah! Nijaalie niwe miongoni mwa wenye kutubia kwako na unijaalie niwe miongoni mwa wenye kutwaharika na unijaalie niwe miongoni mwa waja wako wema. Utukufu ni wako, Ee Allah umetukuka. Nashuhudia kuwa hapana Mola ila wewe. Naomba msamaha wako na natubia kwako.

Maji Safi

Maji safi ni yale yanayofaa kutawadhia au kuondoshea najisi. Maji safi, kwa mfano yakiwa kwenye ndoo au mtungi yanatakiwa:

1. Yasiwe yametumika kwa kufulia, kunawia ama kuoshea vyombo.
2. Yasiwe yameingiliwa na najisi.
3. Yasiwe yamebadilika rangi yake ya asili.
4. Yasiwe yamebadilika harufu yake asili.
5. Yasiwe yamebadilika utamu wake wa asili.



Maji safi yakiwa kwenye ujazo wa pipa (debe 12) au zaidi huhesabika kuwa ni mengi. Maji safi yakiwa mengi

hayaharibiki kwa kufulia au kuogea au kuoshea vyombo ndani yake. Ila huharibika kwa kua na sifa zifuatazo:

1. Kuwa na rangi isiyokuwa asili yake.
2. Kuwa na harufu isiyokuwa asili yake.
3. Kuwa na utamu usiokuwa na asili yake.

Kwa mfano maji ya bahari ya chumvi lakini yanafaa kujitwahaishia kwa sababu yako katika asili yake.

Adhana

Waislamu huitwa kwenye swala kwa adhana. Waislamu wanaposikia adhana husimamisha kazi na shughuli zao zote, kisha huelekea msikitini.

Meneno ya adhana

<i>Allah ni mkubwa (mara mbili)</i>	اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ
<i>Allah ni mkubwa. (mara mbili)</i>	اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ
<i>Nashuhudia kuwa hapana Mungu wa haki ila Allah. (mara mbili).</i>	أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ
<i>Nashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah. (mara mbili)</i>	أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ
<i>Njoo kwenye swala (mara mbili)</i>	حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ
<i>Njoo kwenye kufuzu. (mara mbili)</i>	حَيَّ عَلَى الْفَلَاحِ
<i>Allah ni Mkubwa (mara mbili)</i>	اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ
<i>Hapana Mungu wa haki ila Allah.</i>	لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Iqama

Pakikimiwa Waislamu husimama tayari kuanza swala. Tunakimu kwa kusema:

<i>Allah ni mkubwa (mara mbili)</i>	اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ
<i>Nashuhudia kuwa hapana Mungu wa haki ila Allah.</i>	أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ
<i>Nashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.</i>	أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ
<i>Njoo kwenye swala. Njoo kwenye kufuzu</i>	حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ حَيَّ عَلَى الْفَلَاحِ
<i>Swala ipo tayari (mara mbili)</i>	قَدْ قَامَتِ الصَّلَاةُ
<i>Allah ni Mkubwa (mara mbili).Hapana Mungu wa haki ila Allah.</i>	اللَّهُ أَكْبَرُ اللَّهُ أَكْبَرُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Kuswali

Muislamu akiswali huelekea Qibla. Hutia nia moyoni kuwa anaswali swala ya adhuhuri au alasiri au Magharibi au Isha au Asubuhi. kisha huendelea:

1. Kuhirimia swala kwa kusema



1. Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwenye Kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

2. Sifa zote njema zinamstahikia Allah. Bwana na mlezi wa viumbe vyote.

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

3. Mwingi wa Rehma, mwenye kurehemu.

الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

4. Mwenye kumiliki siku ya malipo.

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ

5. Wewe tu ndiye tunayekuabudu, na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

6. Tuongoze katika njia iliyonyooka.

اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ

7. Njia ya wale uliowaneemesha, sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea.

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ
غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ

3. Kurukuu

Kurukuu ni kuinama kwa mbele na kushika magoti pasina kuyakunja. Wakati wa unarukuu utasema:

"Allahu Akbar"

"Subhaana Rabbiyal 'adhwiim"

Utukufu ni wako Ewe Mola wangu uliye mkuu.



رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ

4. Kuitidali

Kuitidali ni kunyanyuka kwenye rukuu na kusimama wima. Wakati wa kuitidali unasema:

"Sami'a Allahu liman hamidah"

Allah anamsikia kila anayemsifu.

"Rabbanaa walakal hamdu"

Ee Bwana Mlezi wetu, sifa zote za ukamilifu ni zako.

5. Kusujudu

Kusujudu ni kuinama kifudifudi na kugusisha chini paji la uso, vijanga, magoti na miguu. Wakati wa kusujudu unasema:

"Allahu Akbar"

"Subhaana Rabbiyal a 'alaa"

Utukufu ni wako ewe Mola wangu uliyetukuka.





اللَّهُ أَكْبَرُ
رَبِّ اغْفِرْ لِي وَرَأْحَمْنِي



وَعَافِنِي وَرَزُقْنِي

7. Sijida ya pili:

Utasema “Allahu Akbar” na kurudia kusema:

“Subhaana Rabbiyal a’alaa

Utakatifu ni wako ewe Mola wangu uliyetukuka.



اللَّهُ أَكْبَرُ
سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى



6. Kikao kati ya sijida mbili

Ni kuinuka kutoka kwenye sijida kwa kusema “Allahu Akbar”. Na kuomba:

Rabbighofir lii warhamnii wa ‘aafinii warzuqnii”

Ee Bwana mlezi Nisamehe na nirehemu, uniondolee adha (kero) na uniruzuku.




اللَّهُ أَكْبَرُ



8. Kukaa Tahiyatu

Ni kuinuka kutoka katika sijida ya mwisho ya rakaa ya pili au mwisho wa sala na kutulia kwa ajili ya kumuamkia Mtume (s.a.w), kutoa shahada na kumsalia Mtume (s.a.w). wakati wa kuinuka kutoka kwenye sijida utasema:

“Allahu Akbar” (Mungu ni Mkubwa)



9. Kusoma Tahiyiyatu

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ، وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ ،

*Attahiyiyatu lillahi, wasswalawaatu,
watwayyibaatu.*

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ،

*Assalaamu 'alaika ayyuhannabiyyi,
waramatullahi wabarakaatuhu.*

وَالسَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ،

*Assalaamu 'alainaa wa 'alaa
'ibaadillahi sswalihinna.*

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

*Ash-hadu al-llaa ilaha illa Llah, wa ash-hadu anna
Muhammadan 'abduhu warasuuluhu.*

Maana ya maneno ya ttahiyiyatu

1. Maamkizi yote na swala zote nzuri ziwe kwa Allah.
2. Amani na Rehema za Allah ziwe juu yako ewe Mtume na baraka zake.
3. Amani iwe juu yetu na juu ya waja wa Allah.
4. Nashuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na Ninashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mtume wa Allah.

10. Kumswali Mtume

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى

إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى

آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ

إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

Allahumma Swallii 'alaa Muhammad, wa-'alaa aali Muhammad, kama sw-swallaita 'alaa Ibrahiima wa-'alaa aali Ibrahiima innaka hamiidun-majiid, wabaariki 'alaa Muhammad, wa-'alaa aali Muhammad kama baarakta 'alaa Ibrahiima wa-'alaa aali Ibrahiima innaka hamiidun-majiid.

Maana ya maneno ya kumsalia Mtume (s.a.w)

Ee Allah! Mrehemu Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyomrehemu Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika wewe Umtukufu na Msifiwa wa haki. Ee Allah! mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim. Hakika wewe Umtukufu na Msifiwa wa haki”.

11. Kutoa Salaam

Salaam ya kwanza kugeuka kulia, na pili geukia kushoto



“Assalaamu alaikum warahmatullah”

Amani na rehema za Allah ziwe juu yenu.

Dua baada ya Swala



لِلَّهِمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَ مِنْكَ السَّلَامُ تَبَارَكْتَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee Allah! Wewe ni Amani. Na kwako ndiko iliko amani. Wewe ndiye Mbariki, Ewe mwenye Utukufu na Heshima.





Zoezi la Tatu

1. Uislamu ujengwa juu ya nguzo ngapi?

Uislamu umejengwa juu ya nguzo.....

2. Orodhesha nguzo za Uislamu kwa kuanzia ya kwanza kwa mfuatano

(i).....

(ii).....

(iii).....

(iv).....

(v).....

3. Kutoa shahada mbili ni kusema.....*wa*

.....

4. Swala tano anazopaswa Muislamu kuswali ni hizi zifuatazo:

(i).....

(ii).....

(iii).....

(iv).....

(v).....

5. Ili Muislamu awe twahara, ni lazima ngozi na mwili wake pamoja na nguo zake ziwe:

(i).....

(ii).....

(iii).....

(iv).....

6. Najisi ndogo ni

(i).....

(ii).....

(iii).....

(iv).....

(v).....

7. Najisi ndogo hutwahirishwa kwa maji safi kwa kuosha sehemu yenye najisi mpaka.....na viondoke.

8. Muoneshe baba, mama au Ustaadh namna unavyoweza kuswali kwa vitendo na maneno mpaka mwisho.

Mtoto Mwema

Kumkumbuka Allah (s.w) kila wakati

Mujtaba ni mtoto wa Kiislamu. Mujtaba ni mtoto mwenye tabia njema kabisa. Humkumbuka Allah (s.w) kila wakati.



Akiamka asubuhi kutoka usingizini humshukuru Allah (s.w) kwa kusema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا
وَأَلَيْهِ النُّشُورُ


Shukrani zote zimemstahiki Allah ambaye ameturejesha katika uhai baada ya kutufisha. Na Yeye ndiye atakayetufufua.

Mujtaba huamshwa na adhana ya al-Fajiri. Baada ya kuamka hupiga mswaki na kutawadha kwa ajili ya swala ya Al-Fajiri.

Mujtaba ni Muislamu. Muislamu huanza kila jambo kwa jina la Allah. Akipiga mswaki husema: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*: Yaani: Kwa jina la Allah mwingi wa rehema mwenye kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Akianza kutawadha husema: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*
Akianza kunywa chai husema: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*
Akianza kwenda shule husema: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*
Akianza kuandika husema: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*



Muislamu huanza kila jambo jema kwa kusema: *Bismillahir Rahmaanir Rahiim*.

Mujtaba hufanya hivi kwa kuzingatia Hadith ya Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) amesema kuwa:

Jambo lolote lile lisiloanzwa na "Bismillaahir –Rahmaanir-Rahiim limekosa baraka za Allah (Rehema ya Allah)".

Mujtaba akitoka nyumbani kwenda shuleni huaga Kiislamu. Husema:

فِي أَمَانِ اللَّهِ

Muwe katika amani ya Allah.

Baba, mama na wadogo zake humuitikia:

فِي أَمَانِ اللَّهِ الْكَرِيمِ

Uwe katika amani ya Allah aliye karimu.



Muislamu akipiga chafya husema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ

Shukrani zote anastahiki Allah.

Na wenzake huitikia:

يَرْحَمَكَ اللَّهُ

Rehema za Allah ziwe juu yako.



Kisha humalizia kwa kusema:

يَهْدِيكُمْ اللَّهُ وَيُصْلِحُ بِالْكَرُمِ

Allah akuongozeni na akunyoosheeni mambo yenu.

Mujtaba humaliza kila jambo jema kwa kumshukuru Allah (s.w) kwa kusema *Al-Hamdulillah*.

Muislamu akianza kulala usiku, hukalia kiganja cha kulia kama alivyotufundisha Mtume (s.a.w). Kisha husema:

اللَّهُمَّ بِاسْمِكَ أَمُوتُ وَأَحْيَا

Ee Allah kwa jina lako ninakufa na kuishi.



Hakika Mujtaba ni mtoto mwema. Humkumbuka Allah kila wakati, kuanzia anapoamka Al-fajiri mpaka anapolala tena usiku.

Sisi ni Waislamu. Hatuna budi kumuiga Mujtaba ambaye huishi kwa kufuata mafundisho ya Mtume (s.a.w).

Maamkizi

Ibrahimi ni mtoto mwema. Akiamka huwasalimia wenzake waliolala pamoja. Kisha huenda kumsalimia baba, Mama na wakubwa zake.

Huwatolea salaam ya Kiislamu. Huwasalimia kwa kusema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

Amani iwe juu yenu na Kenema za Allah na Baraka zake.

Waliosalimiwa huitikia:

وَعَلَيْكُمْ السَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

Nanyi amani iwe juu yenu na rehema na Baraka za Allah.

Ibrahim baada ya kuwasalimia baba, mama na wakubwa zake, humshika mkono kila mmoja na kuwataka hali. Humuuliza kila moja.



Umeamkaje baba? Umeamkaje mama? Umeamkaje kaka?
Umeamkaje dada? Mmeamkaje wadogo zangu?

Ibrahim ana tabia ya kusalimia hata akiwa nje ya nyumbani. Njiani akikutana na watu huwasalimia.

Wakiwa ni Waislamu huwasalimia:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

Wakiwa si waislamu na wakubwa kiumri, huwasalimia **shikamoo**.

Kusalimia ni tabia nzuri inayohimizwa sana katika Uislamu.

Ibrahim akirudi nyumbani kutoka shuleni au chuoni hubisha hodi na kuwasalimia waliopo ndani:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

Baada ya kuitikia, huwauliza hali: Habari za kutwa? Au habari za hapa nyumbani?

Kubisha hodi

Ibrahim akitumwa kwa jirani hubisha hodi. Haingii ndani mpaka aitikiwe na kukaribishwa.

Akibisha hodi mara tatu bila ya kuitikiwa huwatolea salaam waliomo ndani. Wakiwa si Waislamu huwapa shikamoo. Kisha Ibrahim husema lile alilotumwa.

Akitekelezewa haja yake huaga kwa kusema:

Maa salaam

Iwapo si Waislamu, Ibrahim huwapa asante na kuwaambia kwa heri.

Ibrahimu amejifunza utaratibu huu wa kubisha hodi kwenye Qur-an katika aya zifuatazo:



فَإِنْ لَّمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ وَإِنْ قِيلَ

لَكُمْ أَرْجِعُوا فَأَرْجِعُوا هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾

Na kama hamtamkuta mtu yoyote basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa "Rudini", basi rudini; hii ni takaso kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyatenda.

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ فِيهَا مَتَاعٌ

لَكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٢٩﴾


Si vibaya kwenu kuingia majumba yasiyokaliwa, (yasiyofanywa maskani: kama mahoteli, maktaba), (bila kupiga hodi), ambamo humo mna manufaa yenu; na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha. (24:28-29)

Heshima na utii nyumbani

Ibrahim na Maryamu ni watoto wazuri. Wana waheshimu na kuwatii wazazi wao na wakubwa zao.

Wakiitwa na baba au mama au mkubwa yoyote huenda haraka na husikiliza kwa makini walichoitiwa. Wakitumwa huenda haraka na hurudi haraka.

Ibrahim na Maryamu wakitumwa kazi huifanya kwa bidii na kwa moyo mkunjufu. Mara nyingi Maryamu na Ibrahim hujituma kazi wenyewe.



Ibrahim na Maryamu ni watoto hodari na wenye bidii ya kazi. Huwasaidia wazazi wao kazi zote za nyumbani wanazoziweza.

Ibrahim na Maryam wakiongea na wazazi wao hushusha sauti zao. Hawapandishi sauti zao zikawa juu ya sauti za wazazi wao au wakubwa zao.

Huongea nao kwa upole na huruma. Huongea na rafiki kwa sauti ya upendo na huruma.

Ibrahim na Maryamu hushusha sauti zao kwa kuzingatia maelekezo ya Allah yaliyo katika aya ifuatayo:

وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَأَغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿١٩﴾

Na ushike mwendo wa katikati, na uteremshe sauti yako; bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko zote (kwa makelele yake ya bure). (31:19)

Ibrahim na Maryamu wanapofanya kosa lolote huomba msamaha na hawarudii kosa hilo.

Kisha humuomba Allah awasamehe kwa kosa hilo. Qur'an inafundisha watu kumuomba Allah msamaha. Inasema:

وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٠﴾

... Na ombeni msamaha kwa Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu. (73:20)

Ibrahimu huwasalimia wageni na kiume kwa kuwashika mikono.
Maryam naye huwasalimia wageni wa kike kwa kuwashika mikono.



Baada ya kuwapokea wageni na
kuwasalimia, huwakaribisha ndani
na kuwaomba wakae.



Kisha huwafahamisha
mama au baba kuwa kuna
wageni.

Heshima na Utii nje ya nyumbani

Jihaad na Jannat ni watoto wenye utii na heshima hata wakiwa nje ya nyumbani.

Hutembea upande wa kulia mwa barabara.




Huwapisha kwa heshima watu wanaokutana nao. Huwasalimia kwa “Assalaam Alaykum Warahmatullah” kama ni Waislamu.


Ikiwa si Waislamu huwapa “shikamoo” au salaam nyingine iliyozeleka katika sehemu hiyo ambayo haina tafsiri mbaya.

Watoto wa Kiislamu wanapoitwa na wakubwa njiani huwaitikia na kuwasikiliza kwa makini.

Wakikanywa jambo huliacha mara moja. Wakiombwa msaada kama vile kusukuma gari, hutoa msaada kwa moyo mkunjufu.



Watoto wa Kiislamu hawatoi msaada katika mambo mabaya aliyoyaharamisha Allah. Watoto wa Kiislamu hawali huku wakitembea njiani. Wala hawachezi chezi ovyo njiani. Bali hutembea upesi upesi na kufika haraka huko wanakokwenda.



Watoto wa Kiislamu huwaheshimu na kuwatii waalimu wao na viongozi wa shule au chuo. Huwa na hesima na utii wakiwa ndani ya darasa au nje ya darasa. Wakiwa ndani ya darasa, humsikiliza Ustadhi au Mwalimu kwa makini. Hufanya kazi za darasani kwa bidii kama walivyoagizwa na Mwalimu. Wakiwa nje ya darasa, hufanya kazi za shule au chuo kwa bidii.



Watoto wa Kiislamu hawashiriki katika miradi ya shule iliyoharamishwa na Allah (s.w).



Watoto wa Kiislamu huwasaidia walimu wao na viongozi wao wengine wa shule katika mambo mema. Watoto wa Kiislamu hawatawasaidia waalimu na viongozi wengine katika mambo aliyoyaharamisha Allah (s.w).

Huruma

Hamida ni Muislamu. Yuko darasa la saba. Hamida ni mtoto mwenye huruma na upendo. Hukaa vizuri na wadogo zake. Wanapokosea huwaonya na kuwaelekeza vizuri kwa upole. Huwafunza adabu na tabia nzuri. Huwaelekeza vizuri namna ya kukoga vizuri, kufua na kupiga pasi. Pia huwaelekeza namna ya kuvalia Kiislamu.



Huwahimiza kujisomea na kuwasaidia katika masomo yao ya shuleni na chuoni.

Tabia ya Hamida haiishii kwa wadogo zake tu. Bali huwafanyia huruma na upendo watoto wengine.

Hamida pia huwahurumia vilema, vikongwe na mama wajawazito. Akiwa kwenye gari, husimama na kumwachia kiti kikongwe au kilema au mama mjamzito.



Akimkuta njiani mtu aliyeelemewa na mzigo humsaidia kubeba. Hamida yuko tayari kumsaidia yeyote anayehitaji msaada kwa kilele anachoweza.

Hakika Hamida ni mtoto mzuri, mwenye huruma na upendo.

Tabia hii ya huruma ameipata kwa kufuata hadithi za Mtume (s.a.w) zifuatazo:

Wahurumie walio ardhini, na yule aliyepo mbinguni atawamiminia huruma yake". Ambaye hawahurumii watu, pia Allah (s.w) hatamuhurumia.

Ushirikiano na watoto wenzake


Hamida hukaa na watoto wenzie kwa upendo. Huwaheshimu na kuwahurumia wanapokuwa katika matatizo.

Huzungumza nao vizuri. Hapendi kujiingiza katika matatizo. Hapendi kujiingiza katika ubishi na mizozo.

وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ

الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٦٣﴾

Na waja wa Mwenyezi Mungu (anaowapenda ni wenye sifa hizi):- Ni wale wanaokwenda (na kurejea) ulimwenguni kwa unyenyekevu; na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu; (maneno ya) salama. (25:63)



Huwadhania vizuri wenzake na huwazungumza vizuri wanapokuwa hawapo.

Ni mwepesi wa kuwasamehe wanapomkosea na kumuomba msamaha.

Hamida ni mtoto mwema mwenye upendo na ushirikiano na watoto wenzake. Watoto wote wanampenda Hamida.

Hamida ni mwenye kutosheka na kidogo alichu nacho. Hapendi kuomba omba.

Hana tamaa. Hana wivu. Hachukii mafanikio ya wengine bali huyafurahia.



Hamida ni hodari katika kuchagua marafiki. Huchagua rafiki wazuri wenye tabia njema.

Marafiki wa Hamida ni hodari na wenye bidii katika masomo. Pia ni wenye kujiepusha na marafiki wabaya.

Hakika Hamida na marafiki zake ni watoto wazuri sana. Wana tabia njema kabisa.

Hamida amefanikiwa katika kuchagua marafiki kwa kuzingatia maelekezo ya aya ifuatayo:

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَاتَّقُوا

اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢﴾

Na saidianeni katika wema na ucha Mungu wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu, kwa hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu. (5:2)



Zoezi la Nne


1. Muislamu anapoamka kutoka usingizini humshukuru Allah (s.w) kwa kusema.....
2. Muislamu huanza kila jambo jema kwa kusema
3. Mujtaba akitoka nyumbani huwaaga wazazi wake kwa kusema.....
4. Muislamu akimaliza kufanya jambo jema humshukuru Allah (s.w) kwa kusema.....
5. Qur'an inatufunza kuwa, tunapokwenda kwenye majumba ya watu, tunatakiwa:
 - (a).....
 - (b).....
 - (c).....
 - (d).....
6. Muislamu anapogunduwa kuwa amemfanyia kosa mtu au Allah (s.w) huomba
 - (i)..... au na kisha
 - (ii)kwa Allah (s.w)
7. Muislamu anapokutana na watu anaowajua au asiowajua huwasalimu kwa kusema.....
8. Taja tabia njema kumi na tano(15) alizonazo Hamida
9. Taja tabia mbaya tatu ambazo muislamu hatakiwi kuwa nazo.

Mtume Muhammad (s.a.w)

Nasaba ya Mtume Muhammad (s.a.w)

Muhammad (s.a.w) ndiye Mtume wa mwisho. Hatakuja tena Mtume mwingine baada yake.

Mtume Muhammad (s.a.w) alizaliwa katika mji wa Makka, mwezi 12 Mfunguo sita (12 Rabbiul-awwal) sawa na tarehe 20 Aprili 570.



Baba yake Mtume ni Abdullah bin Abdul Muttalib ibn Hashim bin Abdul Manaaf. Baba yake Mtume (s.a.w) alifariki kabla Mtume hajazaliwa.

Muhammad (s.a.w) alipozaliwa babu yake Abdul Muttaalib alifurahi sana. Alimpa jina la Muhammad. Jina Muhammad lina maana ya “Mwenye kushukuriwa kwa vitendo vyake vizuri”.

Babu yake alimtarajia kuwa na cheo hicho cha kushukuriwa na kila mtu.

Mama yake Mtume (s.a.w) ni amina bint Wahhab bin Abdul-Manaf; Baba na mama yake Mtume, wote walitokana na kabila tukufu la Quraish. Quraish ni babu wa mababu wa Mtume (s.a.w).

Quraish ni katika kizazi cha Nabii Ismail (a.s). Nabii ismail (a.s) alikuwa mtoto wa kwanza wa Nabii Ibrahim (a.s), mtoto wa pili wa Nabii Ibrahim (a.s) ni Nabii Is-Haq (a.s).

Hivyo Mtume Muhammad (s.a.w) ni mjukuu wa wajikuu wa Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kwa kizazi cha Nabii Ismail (a.s). Nabii Ibrahiim (a.s) na Ismail (a.s) ndio waanzilishi wa mji wa Makka.

Mitume hawa ndio waliojenga upya Ka'abah kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ

مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

Na Ibrahim alipoinua kuta za nyumba hii ya Ka'abah) na Ismail. (Kisha wakaomba wakasema):

Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga Ka'abah). Hakika wewe ndiye Mwenye kujua mwenye kusikia. (2:127)

Ka'abah ni msikiti mtakatifu wa Allah (s.w) uliojengwa tangu wakati wa Nabii Adam (a.s), mtu na Mtume wa kwanza. Tunajifunza katika Qur-an:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿٩٦﴾

Kwa yakini nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu ni ile iliyoko Makka yenye baraka na uongozi kwa ajili ya walimwengu wote. (3:96)

Baada ya muda kupita nyumba hii ilibomoka ndipo Nabii Ibrahim (a.s) na mtoto wake wakapewa amri na Mola wao kuijenga upya juu ya msingi wake ule ule.

Mji wa Makka umepata utukufu kutokana na Ka'abah. Pia kabila la Quraosh limepata utukufu kutokana na jukumu lake la kuitunza Ka'aba. Turejee Suratul Quraish:

Suratul Quraysh

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah (s.w) mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ قَرِيشٌ ۝١

1. Ili kwuafanya Makurayshi waendeleo.

إِلْفِهِمْ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ۝٢

2. Waendeleo na Safari zao za wakati wa kusi (kwehda Yemen) na wakati wa kaskazi (kwenda Shamu).

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ۝٣

3. Basi nawamuabudu Bwana wa nyumba hii (Al-Kaaba).

الَّذِي أَطَعْتَهُم مِّنْ جُوعٍ ۝٤ وَأَمَّنَّهُم مِّنْ خَوْفٍ ۝٥

4. Ambaye anawalisha (wakati Waarabu wenzao wamo) katika njaa, na anawapa amani (wakati wenzawao wamo) katika khofu.

Malezi ya Mtume (s.a.w)

Amina alimnyonyesha mwanae kwa muda wa siku saba tu baada ya kuzaliwa kwake. Haikuwa tabia ya wanawake wa kabila la Quraish kuwanyonyesha wenyewe watoto wao. Ilikuwa ikionekana ni aibu kufanya hivyo. Hivyo baada ya siku saba Muhammad (s.a.w) alinyonyeshwa na mjakazi aliyelitwa thuwayba. Mjakazi huyu alitolewa na ami yake abu Lahab bin Abdul-Muttalib. Thuwayba alimnyonyesha Muhammad (s.a.w) mpaka kufika msimu wa kuja wanyonyeshaji.

Wanyonyeshaji walipoingia Makka, walisita kumchukua Muhammad (s.a.w) kwa kuwa alikuwa mtoto yatima. Walihofia kuwa hawatalipwa vizuri. Baadaye mama mmoja aitwaye Halima binti Abi Dhuayb alimchukua Mtume.

Bibi Halimah alitokana na kabila la bani Hawazin lililoishi karibu na mji wa Taif. Taif iko kilometa 96 mashariki ya Makka. Maquraishi walipendelea sana watoto wao wanyonyeshwe na wanawake wa kabila la Bani Hawazin kwa sababu tatu zifuatazo:

- (i) Sehemu za Taifa zilikuwa na hewa nzuri.
- (ii) Wanawake wa Bani Hawazin walikuwa nadhifu.
- (iii) Bani Hawazin walikuwa wakizungumza Kiarabu fasaha.

Bibi Halima alimnyonyesha Mtume kwa miaka miwili. Kwa kuwa Makka palikuwa na magonjwa ya watoto ya kuambukiza, Abdul-Muttalib alimuomba bibi Halima aendelee kumlea mtume (s.a.w) kwa miaka mingine miwili.

Mtume alirejeshwa kwa mama yake mzazi alipokuwa na umri wa miaka minne. Mtume alipofikia umri wa miaka sita mama yake alifariki. Malezi ya Mtume yakawa chini ya Babu yake ambaye ni Abdul Muttalib. Alipofikia umri wa miaka minane, babu yake alifariki. Baada ya kufa Abdul-Mutwalib malezi ya Muhammad (s.a.w) yalikuwa chini ya ami yake, Abu Talib in Abdul-Muttalib.

Tabia ya Mtume (s.a.w)

Tangu udogoni mwake Muhammad (s.a.w) aliondokea kuwa na tabia nzuri sana. Alimzidi kila mtu kwa tabia nzuri. Kila tabia njema iliyosifiwa katika Qur-an alikuwa nayo tangu udogoni mwake. Siku moja bibi Aysha aliulizwa: “Tabia ya Mtume ilikuwaje”? Aysha alijibu: “Tabia yake ilikuwa kama inavyoelezwa katika Qur-an:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

“Na bila shaka una tabia njema kabisa”. (68:4)

Muhammad (s.a.w) tangu utotoni mwake alikuwa mkweli, mwaminifu, mwadilifu, mpole, mwenye huruma, mkarimu, mwenye haya, mwenye kila sifa mzuri zinazopendeza kwa binaadamu wenzake na Mola wake.

Muhammad (s.a.w) hakuwahi katika maisha yake kusifika kwa tabia mbaya. Hata alipokuwa mtoto hakushiriki katika michezo ya upuuzi.

Hakupata kuabudu masanamu, kucheza kamari wala kudhulumu haki ya mtu yeyote. Mtume mwenyewe alikuwa akisema:

“Sikupata kufanya hata siku moja yale mambo waliyokuwa wakifanya makafiri”.

Watu wote wa Makka walikuwa wakimsifu Muhammad (s.a.w) kwa tabia yake nzuri. Hata wakampa jina la **al-amin** – Mwaminifu.

Wakubwa na wadogo walikuwa wakimheshimu na wakimpa amana zao awawekee. Pia alikuwa mkweli mno. Alipewa jina lingine la Assadiq – Mkweli. Majina mawili haya yalikuwa maarufu sana. Watu wote wa Makka walimuita **Assadiq Al-amini**.

Muhammad (s.a.w) alipokuwa na umri wa miaka ishirini, alijiunga na chama cha kuwatetea na kuwasaidia wanyonge wa Makka na kulinda haki zao.

Kazi yake ya Uchumi

Muhammad (s.a.w) alifanya kazi alizoziweza kuwasaidia walezi wake. Kazi kubwa aliyofanya katika utoto wake ni kuchunga mifugo ya familia yake na ya jirani zake.

Mtume alipokuwa na umri wa miaka tisa aliongozana na Baba yake mdogo Zubair kwenye msafara wa biashara. Safari hii walienda Yemen. Alipotimia umri wa miaka 12 aliongozana na mlezi wake Abu Talib, kwenye msafara wa biashara kwenye Sham.

Alipotimia umri wa miaka 15 alianza kufanya biashara mwenyewe katika misafara ya miji iliyokaribiana na Makka. Alipata sifa kubwa katika kazi hii ya biashara kutokana na uaminifu na ukweli wake katika biashara.

Muhammad (s.a.w) kuajiriwa na bibi Khadija

Palikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa tajiri sana katika mji wa Makka. Mwanamke huyo aliitwa Khadija binti Khuwaylid. Khadija alikuwa na kawaida ya kukodi watu kumpelekea bidhaa zake Yemen na Sham (Syria).

Katika msafara mmoja wa Yemen alipokuwa anatafuta mtu wa kumpelekea bidhaa zake huko, Abu Talib alimfahamisha Khadija kuwa Muhammad yuko tayari kwa malipo ya ngamia wawili.

Khadija, alikubali haraka haraka kwa kujua sifa zake. Muhammad alifanikisha msafara wa Yemeni na kurejea na faida kubwa zaidi kuliko matarajio ya Khadija. Jambo hili lilimpendeza sana Khadija ikabidi amkodi tena Muhammad kwa msafara wa Sham kwa malipo mara dufu. Muhammad alikubali na alimletea Khadija faida kubwa sana kuliko alivyotarajia.

Pia bibi Khadija alipata taarifa nzuri juu ya tabia nzuri ya Muhammad kutoka kwa Mtumwa wake Maysara waliyeongozana naye. Kutokana na haya bibi Khadija alimpenda sana Muhammad.

Alimwomba amuo kupitia kwa shoga yake Nufaysah. Wakati huo Khadija alikuwa na umri wa miaka 40 na alishaolewa mara mbili na kuzaa watoto watatu (3). Muhammad (s.a.w) alikua na umri wa miaka 25 na alikuwa bado hajaoa.

Mtume alisita kumuoa Khadija kwa kuwa hakuwa na mahari ya kumpa. Khadija alimtolea mahari ya ngamia 40. Basi Muhammad alikubali na wakaoana.

Kuamua ugomvi

Mtume alipokuwa na umri wa miaka 35 ikaonekana kuna haja ya kujenga Ka'aba upya baada ya kutokea ufa mkubwa. Makabila yote ya Makka yalipewa kazi maalum katika ujenzi huu. Ikabakia kazi ya kuliweka jiwe jeusi (Hajar-al-aswad) mahali pake.

Ukazuka mzozo mkubwa kwani kila ukoo ulidai kuwa ndio unaostahiki kupewa heshima hiyo ya kuliweka jiwe jeusi. Hatimaye wote wakakubaliana kuwa Muhammad awe ndiye msuluhishi wao. Muhammad akawasuluhisha kwa hikma kubwa. Aliliinua jiwe hili na kuliweka katika nguo yake. Halafu akamwomba mkuu wa kila ukoo ashike sehemu ya nguo hiyo na kwa pamoja wakaliinua jiwe hilo hadi kwenye Ka'aba. Kisha Muhammad akaliweka mahali pake na wote wakaridhika na ugomvi ukesha.

Muhammad katika Jabal-Hira

Alipofikia umri wa miaka 38 Muhammad hakuweza tena kuvumilia kuona maovu na machafu yanaendelea kufanyika mjini Makka. Alifurahia ziadi kukaa peke yake kuliko kuyashuhudia maovu hayo. Alipata mahali pazuri pa kukaa kwa utulivu. Mahali hapo palikuwa katika pango la mlima Hira lililopo Kaskazini mwa Makka umbali wa kilometa 5 kutoka mji wa Makka.

Kwa muda wa miaka miwili alikuwa akikaa huko kwa muda wa vipindi virefu na kurejea nyumbani mara moja moja kumwona mkewe na watoto wake na kuchukua masurufu. Aliendelea kufanya hivyo hadi alipofikia umri wa miaka 40 ambapo alipewa utume.





Zoezi la Tano

1. Muhammad ni Mtume wa ngapi?.....
2. Mtume wa kwanza anaitwa.....
3. Muhammad alizaliwa mjini....., tarehe 20 April.....
4. Baba yake Muhammad anaitwa.....bin.....bin.....
5. Mama yake Muhammad anaitwa.....bint.....bin.....
6. Jina la Muhammad lina maana ya.....
7. Taja kazi alizofanya Muhammad utotoni mwake na kabla hajaanza kwenda Jabal-Hira.
8. Muhammad (s.a.w) alinyonyeshwa na kulelewa na wanawake wafuatao:
 - (i).....
 - (ii).....
 - (iii).....
9. Muhammad alisifika kwa tabia njema zifuatazo:
 - (i) Mkweli
 - (ii).....
 - (iii).....
 - (iv).....
 - (v).....
 - (vi).....
10. Muhammad (s.a.w) alipewa utume akiwa na umri wa miaka mingapi?
11. Jina la mke wa kwanza wa Mtume Muhammad (s.a.w), ambaye pia ni mama wa waumini ni.....bint.....